



CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA
S. L. P. 35928, DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu: +255 22 2401581, Nukushi: +255 22 2401582
Barua Pepe: tthuhq@tthu.or.tz Tovuti: www.tthu.or.tz

Tarehe: 26/07/2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mwenyekiti THTU Taifa anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wataanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi kama ifuatavyo;-

1.0 CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU ZA JUU TANZANIA (THTU)

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya juu Tanzania (THTU) ni miongoni mwa vyama vya wafanyakazi vilivyopo nchini kikiwa kimepata usajili Na. 23 mnamo tarehe 12/12/2008. Kwa mujibu wa katiba yetu, THTU inajumuisha wafanyakazi wa vyuo vikuu, Vyuo vikuu vishiriki (Umma na Binafsi) na Taasisi za Elimu ya Juu zisizo Vyuo Vikuu, Pamoja na mamlaka zinazofuatilia ubora na maendeleo ya elimu nchini Tanzania.

2.0 KATIBU MKUU – NAFASI 1

2.1 Sifa za Mwombaji

- i. Mwombaji anatakiwa awe na shahada ya Uzamili (Master Degree) au Stashahada ya Uzamili (Postgraduate Diploma) katika moja ya fani zifuatazo; Law (Sheria), Mediation and Arbitration (Usuluhishi na Uamuzi), industrial/Labour Relations (Mahusiano Kazini), Development Studies (Taaluma za maendeleo), Human Resource Management (Menejimenti ya Rasilimali watu) au sifa linganifu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- ii. Awe mwenye Shahada ya kwanza katika moja ya fani zifuatazo; Industrial/Labour Relations (Mahusiano Kazini), Law (Sheria), Development Studies (Taaluma za maendeleo), Human Resource Management (Menejimenti ya Rasilimali watu) au sifa linganifu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Awe na uzoefu wa kazi katika ngazi ya Menejimenti ya vyama vya

wafanyakazi kwa muda usiopungua miaka mitano (5).

iv. Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta vizuri.

3.0 KAZI NA MAJUKUMU:

- i. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Chama katika masuala yote yahasuyo Chama;
- ii. Atasimamia masuala yote ya nidhamu za watumishi walio chini yake;
- iii. Ataandaa na kusimamia ya bajeti ya Chama;
- iv. Atasimamia mapato na matumizi ya Chama;
- v. Atakuwa Katibu wa Vikao vyote vya Chama;
- vi. Atandaa taarifa kila robo mwaka ya utekelezaji wa shughuli zote za Chama;
- vii. Atakuwa Msimamizi wa rasilimali za Chama;
- viii. Atakuwa Msimamizi Mkuu wa masuala ya kiutawala na uratibu wa shughuli za Chama;
- ix. Atasimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Chama;
- x. Atafanya shughuli za utetezi wa haki na maslahi ya wanachama/wafanyakazi kwa mujibu wa Katiba ya Chama;
- xi. Atatunza kumbukumbu zote za Chama;
- xii. Atafanya kazi zozote atakazopangiwa na Mwajiri wake.

4.0 NGAZI YA MSHAHARA NA MUDA WA AJIRA

Mshahara utakuwa kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa THTU. Hali kadhalika, ajira itakuwa ya mkataba wa miaka mitano (5) na marejeo ya kipindi cha miaka mitano mingine endapo utendaji wake utaridhisha.

5.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 50.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma na ujuzi.
- v. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vi. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", Hati Matokeo za Kidato cha Nne na Sita, yaani FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.
- vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 23 Agosti, 2021 saa 10:00 jioni.
- viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kupitia barua pepe (email) ifuatayo:

Barua Pepe: mwenyekiti@thtu.or.tz

IMETOLEWA NA:



Dkt. Paul L. Loisulie
Mwenyekiti THTU Taifa